

## UHAULISHAJI TEKNOLOJIA

Inasimamiwa na mratibu wa uhalishaji teknolojia na mahusiano Majukumu; ni usambazaji wa matokeo ya utafiti wa teknolojia za kilimo, ubunifu na mbinu za kilimo bora kwa wakulima na wadau.

## VIPAUMBELE VYA UTAFITI

Kati ya vituo 17 vya TARI, Kituo kimepelewa jukumu la kufanya tafiti kwenye mazao matatu. Mazao hayo ni Mahindi, Maharage na Viazi mviringo. Lakini Kituo kinafanya pia utafiti wa mazao mengine kama Ngano, Matunda (parachichi).

Pia Kituo kina shamba la chai ambalo ni muhimu katika kukiongezea kituo mapato, kutoa ajira kwa jamii inayozunguka kituo na kuchangia ukuaji wa uchumi wa viwanda kwa kutoa malighafi kwa viwanda vinavyotengeneza majani ya chai.



WASILIANA NA TARI KUPITIA  
MENEJA

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO  
TARI KIFYULILO  
S.L.P 93 MUFINDI  
IRINGA

SIMU: 0765176040/0769492549  
Baruapepe: [cmkifyulilo@tari.go.tz](mailto:cmkifyulilo@tari.go.tz)  
Tovuti: [www.tari.go.tz](http://www.tari.go.tz)

## TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI - KIFYULILO)





### **UTANGULIZI**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ilianzishwa kwa sheria ya Bunge Na.10 ya Mwaka 2016. TARI inatekeleza majukumu ya utafiti wa Kilimo Tanzania Bara, ikiwa chini ya Wizara ya Kilimo. TARI inajumla ya vituo vya utafiti 17 ikiwemo TARI-Kifyulilo.

### **DIRA**

Kuwa Taasisi mahiri ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Bara na Kimataifa.

### **DHIMA**

Kugundua na kuhimiza matumizi ya teknolojia mbalimbali za kilimo ili kuongeza tija, uhakika wa chakula na lishe, kuwa na kilimo endelevu na chenye kuharakisha ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kushirikiana na wadau wa kilimo wa kitaifa na jumuiya ya Kimataifa.

### **MISINGI YA KIMAADILI**

Uwazi; Uwajibikaji; Uadilifu; Weledi; Umahili; Usawa na Ushirikishwaji.

### **MAHALI KILIPO KITUO**

TARI-Kifyulilo inapatikana Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Mufindi, Kata ya Kasanga Kijiji cha Udumuka, Kitongoji cha Idetero Kituo kinapatikana katika mwinuko wa Mita 2,000 kutoka usawa wa bahari. Longitudo 35020'E na Latitudo 080 42'S. Kituo kipo umbali wa Km 150 kutoka Iringa, Km 33 kutoka Nyololo, Km 60 kutoka Mafinga na kutoka Mbeya ni Km 260.

### **HALI YA HEWA**

Wastani wa mvua kwa mwaka ni 1000-1500mm na wastani wa Joto ni 9°C-20°C

### **ENEOLA KITUO**

Kituo kinajumla ya Eneo la Hekta 220 ikiwa 146 hekta zina miti ya asili, miti dawa na miti ya mbao, hekta 32 ardhi inayofaa kulimwa, Hekta 35 zimepandwa Chai, na Hekta 7 kuna Miundombinu ya Barabara na Makazi ya watu.

### **MAJUKUMU YA KITUO**

- Kutafiti, Kusimamia, Kuratibu na kuhamasisha utafiti wa kilimo nchini
- Kushauri Serikali juu ya uandaaji wa sera, sheria na mifumo yote inayohusiana na udhibiti yenye lengo la kukuza na kuimarisha ubora wa utafiti wa kilimo.
- Kuhamasisha uzalishaji na usambazaji wa mbegu za mazao ya Kilimo;
- Kutoa huduma za ushauri kuhusu utafiti, mafunzo, upashanaji na usambazaji wa taarifa za kilimo na sayansi shirikishi;
- Kushirikiana na wadau muhimu wa kilimo kuratibu na kutekeleza vipaumbele vya utafiti wa kilimo hapa nchini;

- Kuandaa viwango vya ubora wa utafiti, miongozo kanuni za maadili, mwenendo wa utoaji huduma za utafiti wa kilimo;
- Kuanzisha na kuimarisha mfumo thabiti na bora wa uhifadhi nyaraka za utafiti wa kilimo, kushirikiana na wadau kukuza na kubadilishana taarifa za utafiti wa kilimo hapa nchini;
- Kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuboresha shughuli za utafiti wa kilimo nchini
- Kufanya kazi nyingine zinazohusiana na utafiti wa kilimo ili kufanikisha utekelezaji wa sheria ya TARI

### **UONGOZI WA KITUO**

#### **MENEJA WA KITUO**

Ndiye mtendaji mkuu wa kituo ana majukumu ya kupeleka mbele Dira na Dhima ya TARI kupitia utekelezaji wa miongozo na mifumo yakiutawala ya taasisi. Wasaidizi wa Meneja wa kituo ni pamoja na Mratibu wa Utafiti na Ubunifu na mratibu wa Uhaulishaji wa teknolojia na Mahusiano.

### **UTAFITI NA UBUNIFU**

Idara inasimamiwa na mratibu wa utafiti na ubunifu Majukumu; kufanya ngunduzi wa teknolojia za kilimo na ubunifu unaozingatia mahitaji ya watumiaji na unaozingatia njia za kisasa za utafiti.